**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Taswira ya Vijana kama Mkakati wa Kuibua Falsafa ya Mwandishi: Tathmini ya Riwaya za G. K. Mkangi Walenisi (1995) na Mafuta (1984)

*Dkt. Naomi Nzilani Musembi, PhD[1*] & Dkt. Peter Karanja, PhD[2]*

[1] Chuo Kikuu cha Sayansi Na Teknolojia cha Jaramogi Odinga Oginga, S. L. P. 210 – 40601, Bondo, Kenya.
[2] Chuo Kikuu cha Gretsa, S. L. P. 3-01000. Thika, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: omisembi@yahoo.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*03 Septemba 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Vijana, Taswira, Mkakati, Falsafa.*

**IKISIRI**

Utafiti unaonyesha kwamba, vijana kote duniani sasa wana utamaduni wao ambao watafiti wanaueleza kama ‘ulimwengu huru’ wa vijana ulio na mitindo na njia za maisha ambazo vijana hufuata ili kujitofautisha na utamaduni wa wazazi wao. Utamaduni wa vijana kwa kiasi kikubwa ni zao la maendeleo katika jamii za ulimwengu. Kadri jamii inavyosonga mbele kimaendeleo, ndivyo ambavyo utamaduni wa vijana unakuzwa, unaimarishwa na kusambazwa miongoni mwa vijana kote duniani. Vijana wamebuni utamaduni wao kama njia moja ya kuasi dhidi ya utamaduni uliotawaliwa na wazee. Wanataka kujihusisha na tabia kama matumizi ya dawa za kulevya, ushoga, uasi wa maadili ya kijamii, mitindo mipya ya mavazi, muziki miongoni mwa tabia nyingine ambazo wanajua huwatenga wazee. Hii ni tabia ibuka ya vijana kupania kuonyesha nguvu na uwezo wao katika jamii. Ujumbe wanaopitisha ni kuwa, hawako tayari kushiriki utamaduni unaowadhibiti na kuwanyima nafasi yao katika jamii. Data ya utafiti huu ilipatikana maktabani ambapo vitabu teule, majarida, tasnifu na maandishi muhimu yanayohusiana na mada ya utafiti yalisomwa na data ya msingi na upili kunukuliwa. Makala hii iliongozwa na malengo mawili. Moja kudadavua taswira mbalimbali za vijana katika riwaya teule na ya pili kubainisha falsafa ya mwandishi Mkangi kupitia taswira ya vijana katika riwaya hizi mbili Makala hii inapanga kuangazia taswira ya vijana wa kisasa katika riwaya ya Mafuta na Walenisi ili vijana waweze kuzinduka na kubadilisha hali yao ya kimaisha. Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kwamba, Matumizi mbalimbali ya taswira kuhusu vijana yanamwezesha Mkangi kuibua falsafa yake kuhusiana na suala la vijana katika jamii zetu na wakati huohuo kutaka kuzindua umma mkubwa wa vijana unaolala ili waweze kuamka na kubadilisha hali yao ya maisha katika dunia hii inayobadilika kila uchao.

**APA CITATION**

Musembi, N. N. & Karanja, P. (2024). Taswira ya Vijana kama Mkakati wa Kuibua Falsafa ya Mwandishi: Tathmini ya Riwaya za G. K. Mkangi Walenisi (1995) na Mafuta (1984). *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 386-394. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

**CHICAGO CITATION**

Musembi, Naomi Nzilani and Peter Karanja. 2024. "Taswira ya Vijana kama Mkakati wa Kuibua Falsafa ya Mwandishi: Tathmini ya Riwaya za G. K. Mkangi Walenisi (1995) na Mafuta (1984)". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 386-394. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

**HARVARD CITATION**

Musembi, N. N. & Karanja, P. (2024) "Taswira ya Vijana kama Mkakati wa Kuibua Falsafa ya Mwandishi: Tathmini ya Riwaya za G. K. Mkangi Walenisi (1995) na Mafuta (1984)", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 386-394. doi: 10.37284/jammk.7.1.2181

**IEEE CITATION**

N. N. Musembi & P. Karanja "Taswira ya Vijana kama Mkakati wa Kuibua Falsafa ya Mwandishi: Tathmini ya Riwaya za G. K. Mkangi Walenisi (1995) na Mafuta (1984)", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 386-394, Sep. 2024.

**MLA CITATION**

Musembi, Naomi Nzilani & Peter Karanja. "Taswira ya Vijana kama Mkakati wa Kuibua Falsafa ya Mwandishi: Tathmini ya Riwaya za G. K. Mkangi Walenisi (1995) na Mafuta (1984)". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Sep. 2024, pp. 386-394, doi:10.37284/jammk.7.1.2181.

## UTANGULIZI

Falsafa ni busara iliyofikiwa baada ya mtu au watu kutafakari kwa kina kuhusu jambo lolote la kilimwengu. Ni busara itokanayo na harakati ya kimawazo. Ni mtazamo wowote madhubuti wa mtu kuhusu kipengele chochote cha maisha (Njogu na Chimera, 1999). Mwandishi husimulia tajiriba mbalimbali ambazo zimemkumba au zimeikuza jamii yake. Hili hutokea zaidi ikiwa haamini dhana ya kustaladhi kwa ajili ya kustaladhi peke yake, yaani kutunga kwa kujistarehesha tu. Masimulizi ya mwandishi aghalabu yatatokana na upekuzi na uteuzi wa hali mbalimbali zinazoigusa hisia zake. Upekuzi na uteuzi wa hali zitakazosimuliwa mara nyingi utakuwa umefungamana na falsafa yake kuhusu yale ayaonayo. Baadhi ya waandishi huongozwa na msimamo wa kinadharia ambao huirutubu falsafa yao ya Maisha. Tukumbuke kwamba, ingawa mwandishi huenda akawa na falsafa pana iliyopenya vipengele mbalimbali vya maisha, atakuwa na falsafa nyingine ndogondogo zitakazojitokeza katika maandishi yake. Hizi falsafa ndogondogo ndizo zitakazojenga na kuibaleghesha falsafa yake pana. Falsafa ya mwandishi hutokana na utazamaji wa yale yanayojiri katika jamii yake, kisha akatafakari na kuiandikia. Mtazamo wake utaathiriwa na mazingira yaliyomlea na kumkuza. Mwandishi yeyote hutokana na mazingira Fulani maalum. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kihistoria, kiuchumi, kijamii, kisiasa, na kisaikolojia. Mazingira humwathiri mwandishi kwa namna moja au nyingine na huwa na mchango mkubwa katika kuivyaza tajriba yake. Mazingira haya ni sehemu ya kile kinachojulikana kama muktadha wa kiasili wa kazi ya kifasihi (Wamitila, 2003). Mwandishi Mkangi kupitia riwaya za *Mafuta* (1984) na *Walenisi* (1995) anaonekana kutumia taswira ya vijana ili kuibua falsafa yake kuhusiana na masuala mbalimbali yanayowakumba vijana katika jamii yake.

Kupitia riwaya hizi, Mkangi anawamulikia vijana masaibu yanayowakumba, chanzo cha Masaibu hayo na wakati huohuo kuwaonyesha njia ambazo wanaweza kutumia ili kujinasua kutoka kwa masaibu hayo. Riwaya za *Mafuta* na *Walenisi* zinafanana. Riwaya zote mbili zinachunguza jinsi mfumo wa kisiasa unaodhibitiwa na tabaka la watu wachache unavyoweza kuathiri maisha ya waliotawaliwa kijamii, kisiasa na hata kisaikolojia. Hizi ni riwaya ambazo zinaonyesha uovu uliopo katika tawala ambazo hazitilii maanani maslahi ya wengi ila zinaendeshwa na kigaro au kikundi cha wachache waliotawaliwa na unyama, ukatili, na udhalimu mkubwa. Kimsingi, tunaweza kusema riwaya hizi mbili ni za ki-itikadi na zinaonyesha msimamo Fulani maalum alionao mwandishi kuhusiana na masuala nyeti yanayoikumba jamii yake yakiwemo masuala kuhusu vijana, na mahusiano ya kijamii-uchumi katika mataifa yetu.

Riwaya hizi mbili zinaonyesha jinsi mfumo uliopo katika jamii zenye dhuluma unavyoundwa ili kuhakikisha wanyonge wanadhibitiwa na kutawaliwa kwa kila njia. Zinaonyesha jinsi jamii

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

zinavyogeuzwa za kingereza na jinsi uhuru wa wengi unavyodhibitiwa na tabaka la matajiri. Hizi ni riwaya zinazoonyesha mateso, dhuluma, na ukandamizaji kwa kina na jinsi jamii inavyopaswa kufanya juhudi za kuhakikisha kuwa udhalimu huo umeondoshwa katika jamii ili maisha yao yawe bora. Hii ni falsafa ambayo Mkangi alipania kuipitisha kupitia kuwasawiri vijana wakiumia na kuteswa na mfumo wa utawala usiowajali ili vijana wazinduke na kubadilisha hali yao ya maisha. Riwaya zote mbili ni za kiukombozi. Ni kielelezo cha jinsi jamii inavyoweza kujinasua kutoka mfumo unaokandamiza na kuwadhalilisha wengi. Riwaya hizi ni za kufikirisha na zinachochea msomaji kijana ajitazame upya na kuichunguza jamii yake kwa jicho pevu na la ndani.

**Usawiri wa Vijana katika Riwaya ya *Mafuta* (1984).**

Riwaya ya *Mafuta* inawasawiri vijana kwa njia zifuatazo ili kuibua falsafa ya mwandishi:

**Vijana ni Wanyonge, Malofa, Wazururaji na Wasio na Kazi**

Vijana wanasawiriwa kama kundi la wanyonge, wasio na kazi, na wanaodhulumiwa na kundi la mapebari wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali katika jamii yao. Usawiri huu wa vijana unaibuliwa kupitia vijana wawili Zuka na Kazamoyo. Mwenye mkunazi anawakilisha baadhi ya mabepari katika jamii wanaomiliki nyenzo za uzalishaji mali. Yeye anaelezwa kuwa mzembe na anatumia vijana kutunda na kumlindia kunazi wakati yeye analala. Aliweza kuwalipa vijana hawa kwa kuwapa kunazi badala ya pesa. Hali hiyo ndiyo iliyowapelekea Zuka, Kazamoyo na wengine kutumia vifuniko vya soda kuchezea Kamari badala ya pesa. Hali hii inaonyesha kwamba maskini hawawezi kufaidika kutokana na mfumo wa kibepari uliopo katika jamii. Taswira ya mwenye mkunazi na vijana wanyonge wasio na kazi anaowatumia kujitajirisha huku yeye akijipumzisha inatuacha na swali moja ambalo ndilo linaibua falsafa ya mwandishi; Mbona mkunazi unamilikiwa na mtu na wengine hawana? Mkunazi hapa unawakilisha njia kuu za kuzalisha mali na mwenye mkunazi anayemiliki njia hizo ni bepari anayeashiria unyonyaji na ukandamizaji wa wengi hasa wafanyakazi. Usawiri huu wa vijana na mwenye mkunazi inaonyesha ukosefu wa usawa katika jamii ya mwandishi. Hali hii inelezwa vizuri na Zuka anaposema;

> *Ni kwa kivipi ni yeye tu ndiye mwenye mkunazi?*
>
> *Inakuwaje ni yeye tu ndiye aruhusiye zitundwe, asipangaye*
>
> *Mafungu ayapaye bei…? Ni yeye ni yeye! Twendeni basi*
>
> *Tukamuulize haya maswali…njiani walijikuta hawako peke yao (uk. 92).*

Maswali anayoyauliza Zuka yanazua zinduko na hapo ndipo falsafa ya mwandishi inapojitokeza. Jambo linalojitokeza kutokana na maswali haya ni harakati dhidi ya ubepari na unyonyaji. Pili, kuna masimulizi yanayoeleza mgawanyiko wa jamii katika matabaka. Kutokana na usawiri wa mwenye mkunazi, baadhi ya migongano ya kitabaka inafichuliwa. Pia, matokeo ya migongano hii yanajulikana. Matokeo haya ni kama wizi, ukosefu wa kazi, na kuwepo na kundi la wazururaji wasiokuwa na lolote la kufanya katika jamii. Mkangi alipania kuwamulikia vijana chanzo cha ukosefu wa kazi, unyanyasaji na wakati huohuo kuwazindua vijana kwamba wanao uwezo wa kuleta mapinduzi ili kubadilisha hali yao ya maisha. Mkangi anawamulikia wasomaji wake kwamba, vijana hulazimishwa kushiriki wizi na mazingira makali ya uchochole wanayoishi. Pili, tabaka la wazururaji linamulikiwa adui wao. Mwenye mkunazi ndiye adui mkubwa wa jamii. Sio wale wanaoshiriki katika wizi wa kunazi zake kama Jali. Falsafa ya Mkangi inajitokeza katika kupinga kumiliki nyenzo za uzalishaji mali na wachache.

Yeye mwandishi kupitia usawiri huu anajitokeza kama mwanaharakati ambaye anataka usawazishaji na ugavi wa mali ya asili na kuondoa ugandamizaji na ukatili. Kutokana na usawiri wa

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

vijana wanyonge, wazururaji na wacheza kamari wasio na kazi, na taswira ya mwenye mkunazi, Mkangi ametumia suluhu ya maandamano ili kubadilisha hali ya vijana. Anamtumia mwenye mkunazi kuashiria chanzo cha baadhi ya matatizo yanayowakumba vijana. Usawiri huu unalenga kuwazindua malofa kuhusu hali yao nyonge wasioitambua. Hii ni taswira inayowabainishia wachochole juu ya hali yao na vile vile kudhihirisha chanzo cha hali hiyo. Usawiri huu unalenga kumchonga msomaji kimawazo ajue kwamba wanaodhaniwa ndio wezi siyo bali ni wale mabepari ndio wezi wa mali ya asili. Kupitia usawiri wa vijana na mwenye mkunazi, Mkangi anatoa wito kwa vijana wapigane dhidi ya unyonyaji katika jamii unaoletwa na mabepari. Hii ndiyo falsafa yake.

**Vijana ni Wanamapinduzi**

Mwandishi anawasawiri vijana kama kundi la wanajamii wenye nguvu ya kuleta mabadiliko katika jamii, kupitia maandamano yanayoleta mapinduzi na uzalishaji wa jamii mpya yenye usawa. Anafanya hivyo kupitia matumizi ya motifu ya safari ya Ti. Baada ya Mtue kutiwa kizuizini, Ti anafunga safari kwenda kutafuta jamii ya Mtue awajulishe msiba uliompata. Safari ya Ti ni ngumu mno na ina matatizo mengi. Ti ni kijana ambaye anapania kuleta mabadiliko katika jamii yake inayokosa usawa. Kutokana na usawiri wa safari ya Ti, Mkangi alilenga kuwazindua vijana kuhusu; kwanza, umuhimu wa kujitolea kupigania mapinduzi yatakayoleta ujenzi wa jamii mpya. Pili, kuwazindua wasomaji kwamba, mtu akiwa na mtazamo wa kimaendeleo na kibinadamu anaweza kusababisha mapinduzi licha ya utajiri wake, kama alivyofanya Ti. Mkangi anaonyesha falsafa yake kupitia usawiri huu kwamba, pamoja na ugumu na mda mrefu ambao mpiganiaji haki huchukua ili haki ipatikane, vita hivi huzaa matunda. Aidha, anawahimiza wanajamii wasife moyo kwani safari huleta mafanikio kama yale yaliyoletwa na safari ya Ti.

**Vijana kama Majeruhi wa Mfumo Mbaya wa Matabaka**

Mwandishi Mkangi anatuchorea taswira ya kuatua moyo mno ya Vijana katika riwaya ya Mafuta akiwa na dhamira ya kuibua falsafa yake kuhusiana na athari ya matabaka katika jamii zetu. Anafanya hivyo kwa kutumia taswira ya kijana kwa jina Matope ambaye anajipata kama majeruhi katika mazingira anamoishi ya ufukara mkubwa. Mateso anayopitia yanasababishwa na mfumo wa kisiasa uliopo katika jamii ambao unajali tu maslahi yao pasipo na kutilia maanani hali ya vijana. Matope ni raia anayeishi katika kidimbwi cha matope kama makazi yake. Jina lake ni la kimajazi linalotangaza sifa za wazi na za kuonekana za mhusika huyu. Anapoletwa mahakamani kutokana na tuhuma ya kuwaosha wateule kwa maji, hulka yake inatisha. Alikuwa amedhulumiwa mno na watesaji wake. Tunaelezwa:

> *...mate aliyotemewa yakiwa sasa yaanza kumdenwa ute, Damu zikimchururuzika, maumivu yakimchoma kama miiba huku mashavu na viungo vikimwira kwa makofi, mateke, bakorana marungu (uk. 43).*

Taswira ya kuonekana ya Matope inaashiria mateso aliyotendewa katika uhalisia wa maisha, kumtemea binadamu mate ni kitendo cha kutomdhamini kama binadamu. Pia taswira ya damu iliyokuwa ikimchururuzika Matope inaonyesha uyakinifu wa kichapo alichokipata kutoka kwa watesaji wake. Maumivu ya Matope yanalinganishwa na maumivu yampatayo mtu anapochomwa na miiba kuonyesha uchungu wa maumivu yale. Mashavu ya Matope yalikuwa yamevimba na kubadilika rangi kutokana na makofi na mateke. Taswira nzima ya Matope inampelekea msomaji kulengwalengwa na machozi. Ni taswira inayochora hali ya kuchukiza. Pia inazindua msomaji kijana kuhusu mikakati inayotumiwa na watawala kuwadhulumu watawaliwa. Aidha, mitafaruku kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa inaangaziwa. Taswira ya kuonekana ya mateso aliyofanyiwa Matope inampelekea msomaji kufahamu mzizi wa hali yake, na wakati huo huo

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

anapata mwamko mpya wa kubadilisha hali mbaya inayosababishwa na mikinzano ya kitabaka katika jamii. Huu ndio uzinduzi aliodhamiria Mkangi kupitia taswira ya mateso kwa vijana ili vijana waweze kubadilisha hali yao inayowakandamiza. Hii sasa ndiyo Falsafa ya mwandishi kuhusu mateso kwa wanajamii inayosababishwa na watawala walio mamlakani. Falsafa ya mwandishi hapa ni kuwa, jambo hili halihitaji kimya. Linahitaji raia kuungana pamoja na kuyapindua machungu yanayowasakama katika jamii zao.

Mateso ya Matope hayakuwa tu mahakamani bali pia katika jamii ya tabaka la juu. Alipokuwa mahakamani, Matope anaeleza shida zake ambazo zinampelekea msomaji kupata ari na ilhamu ya kutaka kubadilisha hali hio. Maelezo ya shida zake yanachora taswira ya kuonekana ambayo inamzindua msomaji. Matope na wenzake wanalala katika vidimbwi vya matope na wanakula mapipani. Hii ni ishara ya ulitima na umaskini wa kiwango cha juu sana ambayo si ngeni katika jamii ya msomaji. Wateule waliajiri askari ili kulinda chakula kilichotupwa mapipani ili kina yakhe wasiule uchafu huo. Tunaambiwa chakula hiki kilichofunda hung'ang'aniwa na watu, nzi na kombamwiko. Taswira inayoibuliwa na mwandishi kupitia chakula kilichofunda mapipani kiking'ang'aniwa na binadamu na wadudu inalenga kuonyesha vile watawaliwa wamedunishwa na tabaka la matajiri. Madhila 'wenye nacho' wanayoyatendea 'wasio nacho' ni taswira yenye uhalisia katika jamii ya msomaji. Matope ni Jazanda iliyotumiwa na Mkangi kuibua falsafa yake kuhusu udhalimu akilenga kuwazindua wasomaji wake kuhusu mfumo wa kitabaka usio na usawa na ambao unapasa kuondolewa kupitia mapinduzi.

## Taswira ya Vijana katika Riwaya ya *Walenisi*

Mkangi ametumia mbinu ya ukinzano kuibua taswira mbili tofauti za vijana katika jamii ya Dzombo na vijana wa Walenisi. Vijana Walenisi ni kichocheo cha kuibulia falsafa ya mwandishi. Mkangi anatumia taswira zifuatazo za vijana wa Walenisi na vijana katika jamii ya Dzombo (Jamii ya Walenisi) ili kuibua falsafa yake kuhusu vijana;

## Vijana kama Watafiti na Wazalishaji Mali katika Jamii

Mwandishi anawachora vijana kama watafiti na wanaotumia ujuzi wanaopata kupitia elimu kutafiti na kubadilisha hali ya kilimo katika inchi yao. Anafanya hivyo kwa kutumia mbinu ya ukinzano katika kulinganisha vijana jamii mbili kinzani. Jamii atokako Dzombo na jamii ya Walenisi. Vijana Walenisi ni kichocheo cha uzindushi kwa vijana na wasomaji wengine wa riwaya ya *Walenis*i. Jamii ya Walenisi ilijigawa katika marika manne makubwa ambayo yalijulikana kama, rika Dunge (watoto), rika Hirimu (vijana chipukizi), rika Kambi (makamu) na rika Vaya (wazee). Kila rika lilikuwa lina jukumu maalum la kutekeleza kwa jamii nzima. Kila mmoja wa vijana hawa alipata elimu ya kutosha ili kumsaidia kila Muwalenisi kama anavyosema mwandishi:

> *Elimu isiyo na lengo la kumpa mteja uwezo wa kuzalisha*
>
> *Mali hiyo haikuwa elimu… (uk. 110).*

Mwandishi katika kupitisha falsafa yake kuhusu hali ya vijana katika jamii yake ambao wana elimu lakini wanalowela mijini kutafuta kazi anatuchorea taswira ya vijana Walenisi. Tunaambiwa rika Hirimu-pora ambao ni vijana wa makamo ilianzisha utafiti wa hali ya juu katika mradi wowote ambao walikuwa wameamua ili kutumikia taifa. Mwandishi anatueleza kwamba, vijana ndio waliochukua jukumu la kulisha jamii nzima kupitia kilimo cha kufa na kupona. Tunaambiwa huko walenisi walifanya utafiti juu ya hali ya anga, udongo, na magonjwa ya mimea. Majibu ya utafiti huu yalitumika moja kwa moja. Walinyunyizia maji mimea yao na hawakutegemea mvua inayokuja kwa misimu isiyoaminika. Vijana walijitolea kufanya kazi bila usimamizi wa nyapara au mtu yeyote. Marika yao mbalimbali yaliifanyia jamii kazi kulingana na uwezo wao na wakaifukuza njaa katika nchi yao.

Bidii ya vijana wake kwa waume katika kilimo cha kufa na kupona na bila usimamizi inachochea zinduko kwa vijana wasomaji wa riwaya ya

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

*Walenisi*. Vijana hawa walijitolea kutafiti na kutia bidi zao katika kilimo bila kushinikizwa. Tunaelezwa:

> *Mbele yake Dzombo kulisimama bahari ya shamba.*
>
> *Mawimbi ya masuke na masuke ya wimbi, mtama, mpunga*
>
> *Mawele na ngano yalikuwa yakishangilia kwa kutikisa vichwa*
>
> *Vyao hewani. Mahindi nayo yalijiandaa kama askari wanaongojea*
>
> *Kukaguliwa (uk. 113).*

Taswira ya kuonekana ya mimea hii imewasilisha falsafa ya mwandishi kwa mafanikio makubwa. Ukubwa wa shamba la mimea hii ya asili umelinganishwa na bahari. Ukubwa wake unaashiria bidi na kujitolea kwa vijana Walenisi kutokomeza njaa kabisa katika nchi yao. Aidha, falsafa ya mwandishi kuhusu umuhimu wa utafiti wa kina kabla ya kutekeleza jambo lolote inaibuliwa vyema na taswira ya vijana wa Walenisi. Mwandishi vile vile anatwambia kuwa vijana walifanya kazi huku wakiimba nyimbo za kizalendo ili kutiana shime wasichoke kazini (uk. 112).

Kuimba nyimbo wakati wa kazi ni ishara ya kufurahia kazi. Vijana wa Walenisi walifanya kazi huku wakiimba nyimbo na mashairi yaliyokashifu Uchuna na udhalimu wao. Tunaambiwa Dzombo alisikia kwa mbali sauti ya vijana wakiimba kazini alipokuwa anazuru miradi yao ya maendeleo. Alisikia sauti ya kike ikihimiza:

> *Hirimu, bega kwa bega. Shime jasho letu ni ngao na shibe*
>
> *Ujira ni wetu; moyo tusife Wachuna tuwafunike: Shibe tupanue*
>
> *Vijana tu raslimali. Atukataaye alaaniwe! Vijana tu viongozi;*
>
> *Si wa kesho ni wa leo (uk.112).*

Wimbo huu unawasawiri vijana hawa kama wazalendo wa nchi yao. Nyimbo hizi ni kichocheo kikubwa cha uzindushi. Mkangi alilenga kuibua falsafa yake kuhusiana na suala nzima la vijana katika jamii yake kwamba, uzalendo huwasukuma vijana kujihusisha na maendeleo ya nchi kutokana na mapenzi makubwa kwa nchi yao. Vilevile, Mkangi alilenga kuibua falsafa yake kwamba, vijana ni viongozi wa leo sio wa kesho. Aidha, alipania kumulika umuhimu wa kuwajibika kwa vijana kazini kupitia nyimbo. Nyimbo za vijana wa Walenisi wakiwa kazini ni za kimapinduzi. Zinaibua hisia za kimapinduzi za vijana ambao wamekataa kuwa makupe na makapi katika jamii zao. Mkangi alipania kupitisha falsafa yake kuwa, vijana wanaweza kujikomboa kimawazo na wakati huo huo kujitahadharisha kutokana na mifumo inayoendeleza utabaka katika kuzalisha mali.

### Vijana Wamekata Tamaa

Kwa kulinganisha taswira ya vijana wa Walenisi na vijana katika jamii ya Dzombo, mwandishi anatumia mbinu ya ukinzano. Mbinu hii inalinganisha vijana Walenisi na vijana ambao hawana kazi, ni majangili, malofa, malaya na ambao hata wakiwa kazini hawana nidhamu yoyote katika jamii ya Dzombo, na ambayo ndiyo jamii ya mwandishi. Taswira ambayo Mkangi anatuchorea ni ya vijana ambao wamekata tamaa kutokana na hali mbaya ya maisha yao. Vijana katika jamii ya Dzombo hawana kazi. Ni wazururaji na malofa ambao kulingana na utawala wao, zamu yao ya kazi ni kesho si leo. Hali hii inaelezwa na kijana Mtu- Wazo anaposema;

> *Wanaume wao nguvu zao ziliishia katika umalaya,*
>
> *Hawakupewa fursa ya kuzalisha mali kwa hivyo wengi*
>
> *Wao walipevuka kuwa majangili, wakora na kumalizikia*
>
> *Magerezani na kufa huko (uk.107).*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

Taswira ya vijana inayoibuliwa na dondoo hili ni kinyume kabisa na ya vijana Walenisi. Inaonyesha mazingira makali wanamokulia vijana wakati wa utawala wa Wachuna. Vijana wanalinganishwa na nzige na makapi. Mwandishi anasema;

> *… lakini watawala hawakujali uele wa hali hii ambayo iliwageuza*
>
> *Hawa nzige kuwa sawa na makapi tu (uk. 108).*

Nzige ni wadudu ambao wana uwezo wa kula chakula na kufanya uharibifu mkubwa wa mimea. Aidha vijana wanalinganishwa na makapi kuashiria kwamba watawala hawakuona faida yoyote inayoweza kuletwa na vijana ndiposa wengi wakaishia magerezani. Tunaambiwa:

> *Na kama makapi, waliteketezwa kwa moto wa marisau,*
>
> *ulevi na magonjwa ya zinaa kama ukimwi na madawa ya kulevya (uk. 108).*

Taswira hii inafumbatwa vizuri na taswira ya familia ya Dzombo aliyoiacha duniani kupitia 'kifo' chake. Mwandishi anatueleza kwamba, akili ya Dzombo siku moja iliruka hadi kwao Duniani, kwa mkewe Hani na watoto wao watano. Alijua kuwa bila msaada wowote, familia yake ilikuwa ikiteseka pakubwa sana, Tunaelezwa;

> *Aliona (Dzombo) mkewe na watoto wakitimuliwa na kuachwa peupe!*
>
> *Aliona wanawe wakifukuzwa shuleni… Aliona binti zake Chizi na Umazi*
>
> *Wakilazimishwa kupiga umalaya huku wakitokwa na machozi…*
>
> *Aliwaona wavulana wake Tsuma, Munga na Chai wakipevuka kuwa walevi,*
>
> *Wevi, watumwa, majangili, magaidi, magawadi na wazururaji malofa.*
>
> *Watu ambao miili yao itakuja kuwa chakula cha marisasi ya wenye mali (uk. 127).*

Taswira ya vijana katika jamii ya Dzombo inatuelekeza katika falsafa ya mwandishi. Falsafa ya mwandishi kutokana na taswira ya familia ya Dzombo ni kwamba, kutokana na ukosefu wa kazi na kutoshirikishwa kwa vijana katika maendeleo ya nchi, wengi wa vijana hawa wanaishia kujitumbukiza katika wizi, umalaya, ulofa na matumizi ya dawa za kulevya na wengi kutokana na maovu haya, hupatwa na magonjwa ya zinaa kama Ukimwi. Lengo la Mkangi katika kutuchorea taswira nzima ya vijana katika jamii zetu ni kutumulikia kwamba, chanzo cha ukosefu wa kazi kwa vijana kinatokana na itikadi potofu kwamba vijana ni viongozi wa kesho, sio wa leo. Kwa hivyo, wangoje kesho yao ifike wapate kazi. Vijana Walenisi wakilinganishwa na vijana kutoka Duniani kwa Dzombo ambao wengi hawana kazi, na wanagonjea tu kuajiriwa katika maofisi na viwanda vikubwa ni kichocheo cha zinduko kwa vijana wasomaji wa riwaya ya *Walenisi*.

Msimamo wa Mkangi hapa na ambao ndio falsafa yake kupitia taswira nzima ya maendeleo ya kilimo huko Walenisi ni kwamba, kilimo ni shina la maendeleo katika nchi nyingi barani Afrika, Kenya ikiwemo, ingawa kinadharauliwa na vijana wengi. Mwandishi alilenga kuitwaza hadhi ya kilimo ili yeyote aifanyaye kazi hii asiione duni. Hii ni falsafa yake. Kutokana na taswira ya vijana Walenisi, Mkangi anawashauri vijana wajihusishe na kilimo na wasikakawane na kulowela mijini wakitafuta kazi ambazo hazipatikani. Vijana nchini Walenisi walikataa dhuluma na mateso waliyosukumiwa na Wachuna kupitia uzindushi wao. Vilevile, mwandishi alidhamiria kuwazindua wasomaji wake wafahamu kuwa, vijana ni kundi muhimu sana katika jamii na ni lazima wapewe nafasi kutoa mchango wao nchini. Aidha, mwandishi alilenga kupitisha wazo kuwa, baadhi ya maovu na magonjwa yanayowakumba vijana chanzo chake ni ukosefu wa kazi. Falsafa yake hivyo basi ni kuwa, hali ya vijana katika jamii yake ina suluhisho. Mosi, vijana washirikishwe katika maendeleo na mipango ya inchi zao na pili, vijana wajitume kufanya kazi kupitia utafiti wa kina ili kubadilisha uchumi wa nchi zao.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

**Vijana kama Viongozi katika Jamii.**

Mwandishi Mkangi anatuchorea taswira ya vijana wakiwa katika nyadhifa za uongozi kupitia riwaya ya *Walenisi*. Anatusafirisha katika nchi ambayo haina ubaguzi kwa vijana. Vijana sawia na wazee, bila hata ubaguzi wa kijinsia wameshika hatamu za uongozi katika viwanda vikubwa vya kuzalisha mali. Dzombo anapokaribishwa katika kiwanda cha kutengeneza trimi, anashtuka kuona Mtu- Binti Fikrini ndiye mkurugenzi mkuu na ana watu wake kwa waume wanaofanya kazi chini yake. Mtu- Binti Fikirini ni kijana na anaheshimiwa sana katika jamii yake. Anasawiriwa kuwa na busara na hekima kiasi kwamba anasimamia kiwanda cha usafiri wote katika nchi ya Walenisi. Hali hii inaonyesha kuwa Wawalenisi hawakuwabagua vijana hasa wa kike hali ambayo ni kinyume na ilivyokuwa wakati wa Wachuna na katika jamii ya Dzombo ambayo vijana wanatelekezwa katika nyadhifa za uongozi kwa kupitia uongo kuwa, zamu yao ya uongozi ni kesho. Si leo.

Aidha, Dzombo anapopelekwa Mapenzoni ambayo ni Thome kuu ya Walenisi, anapata halmashauri hiyo inaongozwa na wazee kwa vijana, wanaume kwa wanawake (uk. 198). Hali hii inamshangaza Dzombo kwa vile huko kwao duniani, alikuwa amezoea kuona madaraka makuu kama haya yakishikwa na wazee. Dzombo anatwambia kwamba, atokako, katika halmashauri kama hii, kijana akipatikana huko labda awe anawatayarishia wengine chai lakini si kiongozi. Isitoshe, Dzombo anapokwenda kushuhudia kufuzu kwa vijana, anashuhudia idadi sawa ya vijana wa kike na wa kiume kazini. Dzombo hakuona ubaguzi wowote katika inchi hii wa wazee kwa vijana au wa kijinsia. Anashtuka kuona wasichana wakiendesha matingatinga, kuburuta mapipa ya mbolea, na kutengeneza mifereji ya kunyunyizia mimea maji. Kazi hizi za vijana wa kike zinaonyesha taswira ya jamii ambayo haimbagui mwanamke. Hakuna kazi zilizotengewa waume na wake Walenisi.

Wito wa Mkangi kupitia taswira kinzani za vijana hasa wa kike katika jamii ya Dzombo na jamii ya Walenisi ni kwamba, vijana wanapaswa kupewa nyadhifa za uongozi sawia na wazee kwa sababu ni wasomi na wana nguvu za kufanya kazi kwa weledi. Jamii haipaswi kuwabagua kwa misingi ya kijinsia. Hii ndiyo falsafa ya mwandishi kuhusiana na taswira ya vijana Wawalenisi ambao wamejikomboa kutokana na utawala dhalimu ikilinganishwa na taswira ya vijana katika jamii ya Dzombo.

## HITIMISHO

Lengo kuu la mwandishi Mkangi katika kuchora taswira mbili kinzani za vijana Wawalenisi na vijana katika jamii ya Dzombo lilikuwa kuibua falsafa yake kuhusu masuala ya vijana katika jamii yake. Mkangi alilenga kuwazindua vijana ili waweze kufafanukiwa na hali zao, chanzo cha hali hizo na suluhu la matatizo hayo ambalo ni mapinduzi. Mbinu ya ukinzano imetumiwa na mwandishi kulinganisha hali nzuri na mbaya ili msomaji apate uhalisi wa maisha katika jamii yake. Kwa kufanya hivyo, falsafa yake imedhihirika wazi kwamba, jamii mpya haiwezi kujengwa pasi kwanza kuwa na elimu pana na mwamko wa jamii nzima. Mwamko huu unahusisha kutambua misingi na historia ya unyonyaji na kusimama tisti dhidi ya mfumo huo wa kukandamiza jamii hasa vijana. Mkangi alidhamiria kuchora taswira kinzani za vijana ili wasomaji wake hasa vijana wapate ujumbe kwamba, wanyonge hawapaswi kupumbazika na itikadi potoshi inayoendelezwa na tabaka tawala katika mataifa yao. Watambue wanaweza kuyabadilisha maisha yao na kuunda jamii yenye usawa na haki.

## MAREJELEO


Kaui, M. (2008). Usawiri wa Vijana katika Tamthilia teule za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa).

Mkangi, G.K. (1984). *Mafuta*. Nairobi: East African Educational Publishers. Ltd.

Mkangi, G.K. (1995). *Walenisi*. Nairobi: East African Educational Publishers.


 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2181

Njogu, K na Chimera, R ( 1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*. Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Wamitila, K.W. (2003). *Mwongozo wa Walenisi*. Nairobi: Sasa Sema Publication Limited.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.